- Uanzishaji na uendeshaji wa mabwawa makubwa ya kisasa ya kufugia samaki
- Uanzishaji wa mashamba makubwa ya kilimo
- Uanzishaji wa viwanda vya uchakataji na uongezaji wa thamani kwa mazao ya ndizi na viazi
- Uzalishaji wa mbegu bora za mazao
- Ujenzi wa kumbi kubwa za mikutano/sherehe

Aidha, alieleza kuwa kampuni ikianzishwa Halmashauri itaweza kuongeza mapato katika chanzo hicho kipya na faida itakayopatikana kutoka katika kampuni itaenda sambamba na utoaji wa huduma bora za kijamii kwa wananchi na kuweza kujiendesha yenyewe. Pia, alieleza kuwa kampuni hiyo itakuwa inawasilisha taarifa zake katika Halmashauri juu ya utendaji kazi wake.

Kikao kilipokea taarifa hiyo, kilijadili na kuazimia kama ifuatavyo:-

- Wajumbe kwa pamoja waliridhia mapendekezo hayo ya uanzishaji wa kampuni ya RDC MULTI-TRADE COMPANY LTD au RUNGWE INVESTMENT COMPANY LTD, kwa lengo la kuwepo kwa uwezo wa kutoa huduma kwa wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe kwa ufanisi kusudiwa.
- Iliazimiwa kwamba utaratibu ufanyike wa kwenda kujifunza katika Halmashauri ambazo tayari zilishaanzisha kampuni kwa lengo la kuwa na uelewa wa usimamizi na uendeshaji wenye tija kwa Halmashauri kiujumla katika kampuni itakapokuwa imeanza kutekeleza kazi zake.

**DO.NA.49/FUM.04/2021/2022 – OMBI LA KUINGIZA BAJETI YA NYONGEZA (SUPPLEMENTARY BUDGET) KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022, KWA AJILI YA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA ELIMU NA AFYA (TCRP) KIASI CHA TSHS: 1,604,872,379.00**

**i. IDARA YA ELIMU MSINGI**

Afisa Elimu Msingi Wilaya aliwasilisha kwenye kikao maombi ya kutanua vifungu ambapo alieleza kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ilipokea kiasi Tshs: 295,344,759.7 kutoka OR-TAMISEMI na TEA kwa mchangauo ufuatao:-

- Bugoba shule ya Msingi Tsh. 11,872,379.85 – kupitia programe ya COVID -19 (GPE) kwa ajili ya Mfumo wa maji
- Ikukisya shule ya Msingi Tsh. 11,872,379.85 - kupitia programe ya COVID - 19 (GPE) kwa ajili ya Mfumo wa maji
- Katumba II shule ya Msingi Tsh. 80,000,000 - kupitia programe ya COVID - kwa ajili ya ujenzi wa Bweni
- Katumba II Shule ya Msingi Tsh. 90,000,000 (EP4R) – ujenzi wa jengo la Utawala na Madarasa
- Lutete Shule ya Msingi Tsh. 46,600,000(EP4R) – ujenzi wa Madarasa na Vyoo
- Katumba II Shule ya Msingi Tsh. 55,000,000 (TEA) – Madarasa na Vyoo



Scanned with CamScanner

ii. **IDARA YA AFYA**

Kaimu Mganga Mkuu Wilaya aliwasilisha kwenye kikao maombi ya kutanua kifungu cha kiasi cha Tshs: 390,000,000.00, kwa ajili ya mpango wa maendeleo kwa ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya UVIKO -19, kwa mchanganuo ufuatao:-

i. Ujenzi wa jengo la dharula katika Hospitali ya Wilaya Tukuyu (Makandana) kwa Tshs: 300,000,000.00
ii. Ujenzi wa nyumba ya watumishi (3 in one) kwa gharama ya Tshs: 90,000,000.00 katika Hospitali ya Wilaya Tukuyu (Makandana

iii. **IDARA YA ELIMU SEKONDARI**

Afisa Elimu Sekondari Wilaya alikieleza kikao kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe inatarajia kupokea fedha toka Serikali Kuu kiasi cha Tshs: 1,111,872,379.85 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 55 pamoja na uwekaji wa mfumo wa maji na upatikanaji wa vyumba hivyo utakuwa umeondoa tatizo la upungufu wa vyumba vya madarasa uliokuwa unaikabili Halmashauri kwa miaka miwili mfululizo kwa maana ya mwaka 2022 vyumba 29 na mwaka 2023 vyumba 26. Ilielezwa kuwa orodha ya shule zenye upungufu wa vyumba vya madarasa ilipatikana kutokana na maoteo ya ufaulu wa wanafunzi wa darasa la saba 6,868 kwa ufaulu wa 90% na kupelekea upungufu wa vyumba 29 kwa mwaka 2022, na kwa mwaka 2023, kutakuwa na wanafunzi 7,907 na kufanya upungufu wa vyumba 26 kwa ufaulu wa asilimia 90, kama ilivyoainishwa katika jedwali lifuatalo:-

| S/N | SHULE | JUMLA YA UPUNGUFU | UPUNGUFU 2022 | UPUNGUFU 2023 | KIASI CHA FEDHA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | KINYALA | 7 | 4(Kinyala) | 3(Igogwe) | 140,000,000.00 |
| 2 | KIWIRA | 4 | 3 (Lubwe) | 1 (Lubwe) | 80,000,000.00 |
| 3 | UKUKWE | 3 | 2 (Lubwe) | 1 (Lubwe) | 60,000,000.00 |
| 4 | IKUTI | 5 | 3 (Ikuti) | 2 (Kyobo) | 100,000,000.00 |
| 5 | NDANTO | 3 | 2 (Ndanto) | 1 (Ndanto) | 60,000,000.00 |
| 6 | NKUNGA | 3 | 1 (Nkunga) | 2 (Isaka) | 60,000,000.00 |
| 7 | KYIMO | 5 | 2 (Kyimo) | 3 (Kibisi) | 100,000,000.00 |
| 8 | ZIWA NGOSI | 2 | 2 (Ziwa Ngosi) | 0 | 40,000,000.00 |
| 9 | MPUGUSO | 1 | 1 (Mpuguso) | 0 | 20,000,000.00 |
| 10 | MASUKULU | 1 | 1 (Masukulu) | 0 | 20,000,000.00 |
| 11 | IPONJOLA | 3 | 2 (Iponjola) | 1 (Iponjola) | 60,000,000.00 |
| 12 | ITAGATA | 5 | 1 (Itagata) | 4 (Itagata) | 100,000,000.00 |
| 13 | KALENGO | 5 | 2 (Kalengo) | 3 (Kalengo) | 100,000,000.0 |
| 14 | NDEMBELA ONE | 6 | 3 (Ndembela One) | 3 (Ndembela One) | 120,000,000.00 |
| 15 | KISONDELA | 1 | 0 | 1 (Kisondela) | 20,000,000.00 |
| 16 | KAYUKI | 1 | 0 | 1 (Kayuki) | 20,000,000.00 |
| 17 | KISONDELA | Kwa ajili ya mfumo wa maji | | | 11,872,379.85 |
| | **JUMLA** | | | | **1,111,872,379.85** |

Kamati ilipokea taarifa hiyo, ilijadili na kuridhia kutanua vifungu vya fedha hizo. Aidha, wajumbe walishauri mambo yafuatayo:-



Scanned with CamScanner

- Fedha hizo zitumike kama ilivyokusudiwa na usimamizi ufanyike kwa kina kwa kushirikiana na Wataalamu, Waheshimiwa Madiwani na wananchi kwa ujumla.
- Pia, wajumbe waliishukuru Serikali Kuu kwa kutoa fedha hizo kwa ajili ya miradi mbalimbali katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe.
- Ilishauriwa kuwa Kata zote zilizopata fedha kwa wingi kwa ajili ya miradi ya madarasa kwa kipindi kijacho cha kuandaa bajeti yazingatiwe maeneo mengine ambayo hayajapata mgao wa fedha hizo.
- Mkurugenzi Mtendaji Wilaya alitoa maelezo kuwa kwa kipindi hicho inatakiwa pia kuangalia namna ya kujielekeza katika ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule za msingi kwa sababu kuna upungufu wa vyumba vya madarasa 516 kwa kipindi cha miaka 2. Vilevile alishauri kuwa inatakiwa kuanzisha mfuko wa maendeleo ya miradi ya Elimu Wilaya ambapo kutakuwa na suala la mpango wa kuchangia na kile kitakachopatikana kitasaidia katika kutatua changamoto za madarasa.

**DO.NA.50/FUM.04/2021/2022 – KUFUNGA KIKAO**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti kwa ajili ya kufunga kikao. Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa michango yao ya mawazo kwa hoja zilizowasilishwa katika kikao hicho na aliwakumbusha Wakuu wa Idara na Vitengo kutekeleza maagizo yote yaliyotolewa katika kikao. Aidha, aliwasisitiza Wataalam kuwa waadilifu katika kusimamia fedha za miradi zilizotolewa na Serikali ili lengo la kutatua changamoto ya upungufu wa vyumba vya madarasa litimie. Pia, alitoa taarifa kuwa kuna watu walikuwa wanauhujumu msitu wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe na tayari walishakamatwa na mashine zao nazo zilikamatwa hivyo taratibu zingine zinaendelea kufanyika. Aidha, aliwasihi wajumbe wote pamoja na wataalamu kuwa endapo kuna watu watakuwa wanaihujumu Halmashauri taarifa ziwe zinatolewa mapema kwenye ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ili kuweza kufanyiwa kazi kwa uharaka. Kisha alifunga kikao saa 10:34 Jioni.

**MUHTASARI UMETHIBITISHWA NA:-**

| | |
|---|---|
| ....................................... | ....................................... |
| **MHE: MPOKIGWA MWANKUGA** | **BW: RENATUS B. MCHAU** |
| **MWENYEKITI** | **KATIBU** |

**TAREHE** 24/11/2021

Scanned with CamScanner

**MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO CHA TAREHE 21/10/2021, KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE WA JOHN A. MWANKENJA**

**WALIOHUDHURIA**

**A: WAJUMBE**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe: Mpokigwa Mwankuga | Diwani Kata ya Masoko | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe: Samwel Mwinuka | Diwani Kata ya Ndanto | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Samwel Mwakasege | Diwani Kata ya Matwebe | Mjumbe |
| 4. | Mhe: Abraham Mwankenja | Diwani Kata ya Bujela | Mjumbe |
| 5. | Mhe: Lydia Sanga | Diwani Kata ya Ibighi | Mjumbe |
| 6. | Mhe: Emmy Maseta | Diwani V/M Kata ya Kyimo | Mjumbe |
| 7. | Mhe: Saimon Kabuje | Diwani Kata ya Bagamoyo | Mjumbe |
| 8. | Mhe: Moyo Mbamba | Diwani Kata ya Iponjola | Mjumbe |
| 9. | Mhe: Salome Mwakapala | Diwani V/M Kata ya Msasani | Mjumbe |

**B: WASIOHUDHURIA**

1. Mhe: Antony Mwantona — Mbunge Jimbo la Rungwe – Kwa taarifa

**C: WATENDAJI**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Bw: Renatus B. Mchau | Mkurugenzi Mtendaji (W) – Katibu |
| 2. | Bw: Polycarp B. Ntapanya | Afisa Utumishi (W) |
| 3. | Bw: Shujaa Hassan | Kaimu Afisa Mipango (W) |
| 4. | Bw: Victor Mwakapala | Afisa Manunuzi (W) |
| 5. | Bw: Augustino Lawi | Afisa Mifugo na Uvuvi (W) |
| 6. | Bw: Stephen Mbiza | Kaimu Afisa Kilimo,Umwagiliaji na Ushirika (W) |
| 7. | Eng: Anosisye Mwasege | Kaimu Mhandisi wa Ujenzi (W) |
| 8. | Bw: Salum Kilanga | Kaimu Afisa Usafi na Mazingira (W) |
| 9. | Bw: Omary Mungi | Afisa Maendeleo ya Jamii (W) |
| 10. | Bibi: Lydia Mwakatumbula | Mratibu wa TASAF (W) |
| 11. | Bw: Meritus Menshi | Kaimu Afisa Biashara (W) |
| 12. | Bw: Lucas Ndombele | Mweka Hazina (W) |
| 13. | Bw: Mathias Benard | Kaimu Afisa TEHAMA (W) |
| 14. | Bw: Isaya Kitumbika | Kny:Mganga Mkuu (W) |
| 15. | Mwl. Gerald Kifyasi | Afisa Elimu Msingi (W) |
| 16. | Mwl. Yona Mwaisaka | Afisa Elimu Sekondari (W) |
| 17. | Bw: Simon Mutabazi | Kaimu Mkaguzi wa Ndani (W) |
| 18. | Bw: Josephat Haule | Afisa Mapato |
| 19. | Bibi: Janeth Chang'a | Kaimu Mwanasheria wa Halmashauri |
| 20. | Bibi: Mkwaya Songo | Kaimu Afisa Ardhi na Maliasili (W) |
| 21. | Bw: Christopher Nyambaza | Kaimu Afisa Uchaguzi (W) |



Scanned with CamScanner